**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIBONDO KWA MWEZI JULAI 2024


**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule;0754 245 595**

**0628 894 021**

**Makamu wa Mkuu wa Shule;0753 876 247**

**Mhasibu:0769 208 036**

**Shule ya Sekondari Kibondo**

**S.L.P 180**

**Kibondo**


**31/05/2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**
**………..............................................**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**Na. Ya Simu.......................................**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO(5) KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIBONDO ILIYOPO HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBONDO MKOA WA KIGOMA KWA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024/2025 na atasoma tahasusi ya …………

Shule ya Sekondari Kibondo ipo umbali wa Kilometa 03 Mashariki mwa Mji wa Kibondo.Usafiri wa Texi kutoka Stendi kuu ya Mabasi unapatikana kwa nauli ya Shs10,000/= , kwa Pikipiki ni Shs4,000/= na Shs7,000/= kwa Bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 01/07/2024 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 01/07/2024 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 14/07/2024.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

**(Sare ya Darasani)**

a) Kwa wasio waislam: Shati mbili nyeupe za mikono mifupi yenye mfuko upande wa kushoto. Sketi 2 mavazi ya darasani yenye rangi nyekundu na marinda ya shule ya msingi au mkeketo-kitambaa kizito cha suti na iwe ndefu hadi kwenye kisigino(upana wa rinda uwe inch 1.5)

b) Kwa waislam: Rangi ya hijab (juba) ni nyeupe isiyo na urembo(kitambaa cha haruwa).Ianzie kichwani na isizidi eneo la kiuno. Shati nyeupe(aina ya tomato) au nusu kanzu nyeupe yenye mikono mirefu. Sketi 2 mavazi ya darasani yenye rangi nyekundu na marinda ya shule ya msingi au mkeketo-kitambaa kizito cha suti na iwe ndefu hadi kwenye kisigino(upana wa rinda uwe inch 1.5)

**ANGALIZO:** Kwa kipengele (a) na (b) kwenye Sare ya SKETI, unajulishwa kuwa SKETI zinapatikana hapa shuleni ili kuepuka mkanganyiko kwa kuchanganya rangi na hii ni kutokana za uzoefu tulionao.

| SKETI NYEKUNDU | SKETI NYEUSI |
|---|---|
|  |  |

c) Sare ya michezo kwa shule hii ni Track suit (01) yenye rangi ya blue bahari yenye mistari nyeupe pembeni na raba pea moja.
d) Jezi nyeupe (01) yenye strips nyeusi isiyo na kola.
e) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
f) Soksi jozi mbili(2) nyeupe za shule.
g) Sweta 2 zenye rangi nyeusi na shingo ya V mbele.
h) Tai nyekundu yenye michirizi midogo midogo nyeupe.
i) T-shirt ya kijivu hii ni sare ya shule (N.B Fulana hii inapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh15,000/=) ikiwa imechapwa nembo ya shule kwa mbele na nyuma ya T'shirt.
j) Nguo za kushindia 'Shamba Dress'

- Kwa **wasio Waislam**: ni sketi 2 za rangi nyeusi iwe kitambaa kizito, cha suti na iwe ndefu hadi kwenye kisigino.(upana wa rinda uwe inch 1.5).
- Kwa **Waislam**: ni sketi 2 rangi nyeusi iwe kitambaa kizito, cha suti na iwe ndefu hadi kwenye kisigino.(upana wa rinda uwe inch 1.5).
- Rangi ya hijab (juba) ni nyeusi isiyo na urembo.Ianzie kichwani na isizidi eneo la kiuno.(kitambaa cha mpira mpira)

k) Fulana ya kushindia(T'shirt) ya rangi nyekundu shingo ya duara na isiwe na maandishi ambayo ni nzito ijulikanayo kwa jina la MANGA.

**ANGALIZO:** Unashauriwa kwenye Tai uje uzichukulie hapa shuleni kuepuka mkanganyiko wa rangi.

**Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari aina ya Counter book(Quire4)yasiyopungua nane(8)
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka
iii. Vitabu vya masomo ya Tahasusi husika (*rejea orodha imeambatishwa)*

iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator;
vi. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni. Aidha, godoro linapatikana kwa kukodishwa shuleni kwa gharama ya **Shilingi 10,000/=**
vii. Mashuka Jozi 2(pink), blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1.
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita 10) zenye mifuniko kwa matumizi binafsi.
xi. Kila mwanafunzi anapaswa alete kotama(siko) pamoja na brush ngumu ya kusafishia sink la chooni.
xii. Kila mwanafunzi anapaswa kuleta ndoo ndogo(lt 10) kwa ajili ya kufanyia usafi wa mazingira ya shule.
xiii. Kila mwanafunzi anapaswa kuja na **Faili 01 ''FILE FOLDER''** ili afunguliwe taarifa zake binafsi za usajili/Kitaaluma.
xiv. Kwa mwanafunzi asiye na Kadi ya Bima ya Afya ya Taifa(NHIF), mzazi unashauriwa kumkatia kadi hii ya Bima ya Afya.

**ANGALIZO**: Kila Mwanafunzi alete vifaa kulingana na mchanganuo ufuatao;

| TAHASUSI | JEMBEna MPINI wake | REKI | KWANJA | FAGIO(CHELEWA) | FAGIO (BROOM) |
|---|---|---|---|---|---|
| HKL | JEMBE | - | - | CHELEWA | - |
| HGL | JEMBE | - | - | CHELEWA | - |
| HGK | JEMBE | - | - | MOPPER | - |
| HGFa | JEMBE | | | | HARD BROOM |
| HGLi | JEMBE | | | | HARD BROOM |
| HGE | - | - | KWANJA | CHELEWA | - |
| EGM | - | REKI | - | - | MOPPER |
| PCM | - | REKI | - | - | MOPPER |
| PCB | - | - | KWANJA | - | SOFT BROOM |
| CBG | - | - | KWANJA | - | SOFT BROOM |

### 2.2 Michango mbalimbali

**Shule ya Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Fedha Jumla ya Fedha zinazopaswa kulipwa Benki ya NMB kwenye akaunti ya shule yenye Namba 51501000010, yenye jina la Akaunti KIBONDO SECONDARY. Aidha, iwapo utakodi godoro fedha yake pia itapaswa kuwekwa kwenye akaunti hiyo hapo juu.**

**(**Tafadhali ukiwa unaweka fedha benki, andika jina la mwanafunzi kwenye eneo la muwekaji fedha iliyopo kwenye slip ya benki na kisha slip(karatasi) hiyo ya malipo inapaswa mwanafunzi aje nayo shuleni akiwa anaripoti.

**ANGALIZO: Shule haipokei fedha au michango yoyote ikiwa Taslimu ''Cash''**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;


xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu vya Kuja NAVYO**


i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na yatekelezwe vema.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**



**KEMILEMBE BAMUHIGA BAKANAMILA**
**MKUU WA SHULE**
**KIBONDO SEKONDARI**




**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na**

**kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA KWA HATUA YA AWALI UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA KUTUMIA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule : 0754 245 595/0628 894 021**
- **Makamu Mkuu wa Shule : 0753 876 247**
- **Mwandamizi Taaluma : 0759 196 722**
- **Mwandamizi Malezi: 0688 315 095**

## SHULE YA SEKONDARI KIBONDO

## FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

A. **SEHEMU YA MWANAFUNZI**

1. Mimi (Majina kamili) ………………………………………………………………….. Nimekubali kuingia kidato cha …………… katika Shule ya Sekondari Kibondo kuanzia tarehe ……………… hadi nitakapomaliza kidato cha …………… 2. Naahidi kwamba nitatii sheria za Shule na kushiriki katika shughuli zote za shule kikamilifu kulingana na ratiba.

3. Tarehe ya kuzaliwa……………………… Kijiji………………………………….. Tarafa…………………………………….. Wilaya ……………………………….. Shule uliyotoka ……………………………………..Namba yako ya mtihani…………………..

4. Nikimaliza kusoma shule ningependa kufanya kazi ifuatayo ……………………………….

5. Kwa akili zangu timamu nikiwa natoka nyumbani kwenye Likizo iwe fupi au ndefu, sitakuja na simu pia nikiwa kwenye mazingira ya shule kwa kipindi chote sitamiliki simu.

6. Kuwahi shule kwa muda na tarehe zitakazopangwa pindi nitokapo likizo aidha ndefu au fupi.

Sahihi ya mwanafunzi ……………………. ………………………Tarehe ………………………

**B. SEHEMU YA MZAZI AU MLEZI**

1.Mimi(majina kamili)………. ……………………………………………………………. ninakubali mtoto wangu asome katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Kibondo kuanzia kidato cha ……………………hadi atakapomaliza kidato cha ……. Nakiri kukubaliana na sheria,kanuni,kulipa Michango ya shule pamoja na kutompa mwanafunzi simu na nitafuata maelekezo mengine yatakayotolewa na Shule.

2. Jina kamili la Mama ………………………………

Jina kamili la Baba……………………………………………………………………

3. Kazi ya Mama …………………………Kazi ya Baba ……………………………………

4.Anwani ya Mzazi/Mlezi…………………………….
5. Wafuatao ni Ndugu zake ninaowatambua wanaishi hapa Kigoma au Jirani na mkoa huu na wanaweza kumsaidia wakati wa dharura

| Majina kamili | Mahusiano Anakoishi | Simu yake |
|---|---|---|

(i)……………………......... ....…………......……………..................................................
(ii)…………………….......... ………..……….…..... .. ……………………………………
6. Madhehebu ya Dini ya Mtoto ni Lutheran/Katoliki/Anglican/PAG/TAG/ Moravian /SDA/Muislam …………………………………….

7. Ripoti zote za maendeleo ya mwanafunzi ziwe zinatumwa kwa: ………………………………………………………..……………………………………

Saini ya Mzazi/Mlezi ...................................................... ……Tarehe ……………………………

**MEDICAL EXAMINATION FORM FOR KIBONDO SECONDARY SCHOOL**

To be completed by a Medical Officer

……………………………………… (Insert name of the Government Medical Institution)

Name of Student ………………………………… Form ………………… Year……………..

Age……………………………………………………Sex……………………………

Blood count……………………………………………………………………………….

Stool ……………………………………………………………………………………

Urine ……………………………………………………………………………………

T.B:Test…………………………………………………………………………………

Eyes……………………………………………………………………………………

Ears……………………………………………………………………………………

Chest…………………………………………………………………………………….

Spleen …………………………………………………………………………………

Abdomen………………………………………………………………………………

Teeth ……………………………………………………………………………....

Additional information: - (e.g. pregnancy, physical defects, infections, psychological disorder, chronic or family diseases).

……………………………….........................................................................................

……………………………………………………………………………………………

I certify that above pupil is fit to continue with studies in Secondary School for two years.

Name of Medical Officer ……………………………………………. Signature ……………………………………………………………………………………………

Designation ……………………………………………………………………………

Station

& Official Stamp…………………………………... Date ………………………

Sharti mtoto apimwe kikamilifu kabla ya daktari kujaza fomu hii. Ikigundulika kuwa daktari alijaza fomu hii bila vipimo kufanyika, wahusika watachukuliwa hatua za kisheria na za ukiukaji wa haki za binadamu.

**NB:SHULE HAINA UTARATIBU WA CHAKULA MAALUMU KWA WAGONJWA(SPECIAL DIET)**

## OORODHA YA ITABU VYA MASOMO KWA WANAFUNZI AMBAVYO KILA MWANAFUNZI ANASHAURIWA KUJA NAVYO SHULENI

CHEMISTRY.

1. S. Chand: A textbook of CBSE chemistry for class Xi

2. Physical chemistry for Advanced level secondary school students book form five and six: Tanzania institute of education.

3. General chemistry for Advanced level secondary school students book form five and six: Tanzania institute of education

4. Inorganic chemistry for Advanced level secondary school students book form five and six: Tanzania institute of education

5. Organic chemistry for Advanced level secondary school students book form five and six: Tanzania institute of education

BIOLOGY

1. S.CHAND: A Textbook of CBSE Biology for class XI.

2. Glenn and Susan Tode :New understanding biology for Advanced level fourth edition

3. D. J Taylor 3rd or1st and 2nd edition .Biological science

PHYSICS

1. S. Chand :Principle of physics class XI.

GENERAL STUDIES

1. J.Bigirwamungu and Deogratias SM 2012 understanding advanced level general studies.Mikumi publishers Dar es sallam

2. Mbalasa r.f(2011) General studies for advanced level certicate form six afroplus industries , Dar es salaam

3. Kamili (2017)General studies alive , kamili Books and General supplies .Dar es salaam

4. Mbalase R.F (2011). General studies for advanced level certicate, Form five Afroplus industrie, Dr es salaam.

ECONOMICS

1. Economics for advanced level paper I and professional studies: Nyambari Nyangwine

2. Economics for advanced level paper II and professional studies: Nyambari Nyangwine

3. Economics simplified (Revised and update).N.A SALEEMI

4. Modern economics(second edition):Robert Mudida

GEOGRAPHY PAPER 1

1. Principle of physical geography by MONKHOUSE

2. Practional Geography by Colin Bucle.

3. PracticaL Geography for A-level by Francis Mnyawi

4. Africa by J.M Prichard

5. Landforms in Africa- An introduction to Geomorphology by Collin Buckle

GEOGRAPHY PAPER II

1. Human and Economic Geography by Goh Cheng & Morgan
2. Advanced level geography course book by Tanzanian Institute of Education (TIE)
3. An Integrated focal regional study on human and Economic geography Advanced level paper 2 by DT Msabila

ADVANCED MATHEMATICS

1. Conceptual Advanced Mathematics V& VI BY R.L MOYOMBA

2. Pure Understanding

3. Pure Mathematics 1& 2 by Backhouse.

KISWAHILI

1. Nadharia ya lugha – Masuko Christopher

2. Nadharia ya lugha– Nyambari Nyangwine

3. Tafsiri na ukalimani – Bakizi

4. Mitaala ya lugha na fasihi – Gibbe A.G

5. Kiswahili kidato cha tano na sita – Oxford

6. Nadharia ya fasihi – Nyambari Nyangwine

7. KAMUSI YA KISWAHILI SANIFU – TUKI

RIWAYA

1. Vuta N'kuvute – Shafi Adam Shafi

2. Mfadhili – Hussein Tuwa

3. Kufikirika – Shaaban Robert

4. Usiku utakapokwisha – Mbunda Msokile

TAMTHILIYA

1. Morani – Emmanuel Mbogo

2. Kivuli kinaishi – S. Mohamed

3. Nguzo mama – Penina Mhando

4. Kwenye ukingo wa Thim – Ebrahim Hussein.

USHAIRI

1. Chungu tamu – T. Mvungi

2. Kimbunga – Haji Gora Haji

3. Mapenzi Bora – Shaaban Robert

4. Fungate ya uhuru – Mohamed S. Khatibu.

**PROPOSED BOOKS FOR ADVANCED LEVEL**

**ENGLISH LANGUAGE 1**

1. English language for Advanced level………………..Nicholaus Asheri
2. English language for Advanced level ………………..Julius A. Tarimo
3. English language for Advanced level……………….Chomsky Noam
4. English language for Advanced level, for five……...Michael Kadeghe.
5. English language for Advance level………………....Oxford
6. Contemporary English for Advanced level …………Mnyawi.

**ENGLISH LANGUAGE 2**

**LIST OF READINGS.**

**PLAYS**

1. Betrayal in the city………………………...Francis Imbuga
2. I will Marry when I want…………………Ngugi wa Thiongo and Ngugi wa Mirii
3. The Bride…………………………………Austine Bukenya.
4. Lwanda Magere…………………………..Okoiti Omtatah
5. An Enemy of the people…………………..Henrick Ibsen
6. Black Mamba……………………………..John Ruganda.

**NOVELS AND SHORT STORIES**

1. Encounters from Africa…………………………Macmillan publishers Ltd
2. The Beautiful Ones are not yet born…………….Ayi Kwei Armah
3. A man of the people……………………………..Chinua Achebe
4. Divine Providence……………………………... Severine N. Ndunguru
5. The Rape of the pearl…………………………...Magala Nyago
6. Vanishing shadows……………………………..Naminge Kayondo
7. His Excellency the head of state………………..Danny Safo.
8. A season of waiting ……………………………David Omowale

**POETRY**

1. Selected poems…………………………………Institute of Education
2. The wonderful Surgeon and other poems……....Charles Mloka